# CHUO KIKUU CHA NAIROBI

# CHUO CHA USANIFU MAJENGO NA SAYANSI YA UHANDISI

## HATI YA UTOAJI HUDUMA

***Kituo kinachoongoza katika ufunzaji wa ubunifu, uvumbuzi na usanifu***

## DIJABI

Chuo cha Usanifu Majengo na Sayansi ya Uhandisi (CAE) ni moja kati ya vyuo sita vya Chuo Kikuu cha Nairobi. Chuo hiki kinatoa mawanda mapana ya masomo ya kiakademia ikiwa ni pamoja na mipango kumi na nane ya masomo ya shahada ya kwanza, diploma za baada ya shahada ya kwanza, mipango ya masomo ya uzamili na uzamifu. Chuo hiki kina shule tatu na taasisi moja-Shule ya Sayansi ya Uhandisi, Shule ya Mazingira Jengwa, Shule ya Sanaa na Usanifu na Taasisi ya Sayansi ya Nyukilia na Teknolojia. Chuo hiki kinaendelea kuimarisha kimfumo mitalaa yake kwa kuambatana na mienendo na matakwa ya viwanda na maendeleo ya kiteknolojia. Kujitolea kwetu kwa dhati katika utoaji wa huduma bora kumekitwa juu ya utiifu wetu wa utawala wa kisheria, rasilimali ya binadamu yenye ustadi, utendaji kazi wa kujitolea, uwazi, uwajibikaji, haki na utoaji wa huduma kwa wakati ufaao. Ubora katika ufundishaji na ujifunzaji, utafiti na usomi, ushauri na huduma kwa jamii, utawala na usimamizi mzuri wa shirika yatasalia kuwa mambo tunayoyaangazia. Hati hii ya Utoaji Huduma iliyofanyiwa marekebisho ni ahadi ya kujitolea kwa Chuo cha Usanifu wa Majengo na Sayansi ya Uhandisi kutoa huduma ya hali ya juu kwa wadau wetu, wanafunzi, wafanyikazi, washirika wa utafiti, wafadhili na umma wote wa Kenya kwa jumla. Maoni na mapendekezo yenu yatatuwezesha kuboresha utoaji wa huduma katika maeneo yanayohitaji uangalizi, uchunguzi na kujitolea.

**Eng.Prof. B.N.K.Njoroge**

**Mkuu wa Chuo**

**Chuo cha Usanifu Majengo na**

**Sayansi ya Uhandisi**

## UTANGULIZI

Hati hii ya Utoaji Huduma ni ahadi ya kujitolea kwa Chuo cha Usanifu Majengo na

Sayansi ya Uhandisi kutoa huduma ya hali ya juu kwa wanafunzi, wafanyikazi, washirika wa utafiti, wafadhili, wadau wengine na umma wa Kenya kwa jumla.

## RUWAZA

Kuwa Kituo kinachoongoza katika ufunzaji wa ubunifu, uvumbuzi na usanifu

## MALENGO

Kufunza wataalam wa kiwango cha juu katika taaluma za uhandisi, teknolojia na mazingira jengwa kupitia ufundishaji, utafiti na ushauri.

## MAADILI YA KIMSINGI

Kwa kuambatana na Hati ya Utoaji Huduma ya Chuo Kikuu cha Nairobi, haja yetu ya kupania kutoa huduma bora za hali ya juu na kwa wakati ufaao, itaongozwa na Maadili ya Kimsingi yafuatayo; kama yalivyoelezwa katika Mpango ya Kimkakati wa Chuo (2008-2013):

- Kutafuta ubora wa hali ya juu
- Ubadilishanaji huru na wazi wa mawazo
- Utaalam
- Utendaji kazi kwa pamoja
- Uaminifu na uadilifu
- Kujitolea kwa bidii katika kutoa huduma
- Kuimarisha uhifadhi wa utumiaji endelevu wa mazingira
- Ufunzaji kwa njia ya ushauri

## KANUNI ZA UTOAJI HUDUMA

Katika utoaji wetu wa huduma tunaahidi;

- Kuwahudumia wateja wetu kwa heshima, adabu na nidhamu
- Kutoa huduma inayostahili na ifaayo kila wakati
- Kuzingatia utoaji huduma katika misingi ya kimaadili na usawa

- Kudumisha uwazi na uwajibikaji kila wakati
- Kutetea kanuni za haki ya kimsingi kila wakati
- Kudumisha ufaragha unaostahili
- Kutekeleza wajibu wetu kitaalam, kwa shauku na uzalendo

## WATEJA WA CHUO

Wateja wa Chuo ni pamoja na;

- Wanafunzi
- Wafanyikazi
- Wazazi
- Watoaji bidhaa na huduma
- Wanafunzi wa zamani
- Na umma kwa jumla

## WAZAZI NA WADAU

Washirika na wadau wa Chuo wanajumuisha hawa wafuatao miongoni mwa wengine;

- Walipa ushuru
- Wizara ya Elimu
- Tume ya Elimu ya Juu
- Bodi ya Utoaji Mikopo ya Elimu ya Juu
- Wizara na Idara za Serikali
- Washirika wa Utafiti
- Taasisi za Mafunzo
- Washirika wa Miunganisho
- Washirika wa viwanda

- Washirika wa Biashara
- Mtandao wa Elimu wa Kenya [Kenya Education Network]
- Waajiri
- Wafadhili
- Wadhamini
- Vyama vya Wafanyikazi
- Vyama vya Wanafunzi
- Mashirika ya Kitaalam
- Mashirika ya Wanafunzi wa Zamani
- Majirani
- Wadau na washirika wengine

## MATARAJIO YA WATEJA

Wateja wetu wanatarajia utoaji wa huduma mwafaka na ifaayo kama ifuatavyo;

- Mchakato ulio wazi wa kuchukuliwa kwa wanafunzi
- Ufundishaji mkamilifu wa mitalaa iliyoidhinishwa
- Ushughulikiaji wa haraka na wa haki wa matokeo ya mitihani, nakala za matokeo ya mitihani na vyeti
- Uimarishaji wa ufadhili wa utafiti
- Utolewaji wa haraka wa matokeo ya utafiti
- Unadhifu na usafi wa kumbi za mihadhara, maabara, afisi na vifaa vingine
- Uuzaji makini wa huduma za ushauri na utafiti
- Usimamizi wenye uwezo wa kubadilika wa rasilimali ya binadamu
- Mfumo ufaao wa ukadiriaji wa utendakazi
- Mfumo ulio wa haki na adilifu wa kushughulikia kesi za nidhamu

- Michakato ifaayo ya ununuzi wa bidhaa na huduma
- Utambuzi na utoaji shukrani kwa wafadhili na wadhamini
- Kuheshimu Mapatano ya Uelewano yanayohusisha taasisi za utafiti, viwanda na washirika wengine
- Matumizi ya Teknolojia ya Kisasa ya Habari na Mawasiliano [Teknohama]
- Kushirikishwa kwa wanafunzi wa zamani katika usimamizi na ustawishaji wa Chuo
- Mazingira salama na safi katika Chuo
- Ushughulikiaji kwa nidhamu na kwa wakati ufaao wa maswali na maulizo, na
- Ushughulikiaji wa haraka wa wanafunzi na wafanyikazi wanaondoka

## MATARAJIO YA CHUO

Chuo kinatarajia wateja na wadau wake;

- Kutangamana na wafanyikazi wa Chuo kwa heshima na adabu
- Kutoa habari ya kutosha na sahihi ili kuwezesha kushughulikiwa kwa maswali yao kwa usahihi
- Kulipa karo na ada zote kwa haraka
- Kuunga mkono mipango na shughuli za Chuo
- Kuheshimu sheria na taratibu za Chuo Kikuu cha Nairobi na Chuo cha Usanifu wa Majengo na Sayansi ya Uhandisi
- Kutoa majibu, maoni na mapendekezo juu ya huduma zinazotolewa

## HUDUMA ZA USAIDIZI

Licha ya afisi nyingi zilizoko katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo cha Usanifu wa Majengo na Sayansi ya Uhandisi katika usimamizi ufaao wa shughuli zake, kina huduma nyingi za usaidizi zinazotolewa na;

- Afisi ya Mkuu wa Chuo
- Afisi ya Msarifu wa Chuo

- Afisi ya Mkuu wa Shule ya Sayansi ya Uhandisi
- Afisi ya Mkuu wa Shule ya Mazingira Jengwa
- Afisi ya Mkurugenzi wa Shule ya Sanaa na Usanifu
- Afisi ya Mkurugenzi wa Taasisi ya Nyukilia na Teknolojia
- Afisi ya Naibu Mshauri Mkuu wa Wanafunzi

## AHADI YA KUJITOLEA KUTOA HUDUMA

- Chuo kitajitolea kikamilifu katika kuwawezesha wanafunzi waliochukuliwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi kupata barua zao za mwaliko miezi miwili kabla ya tarehe ya kuwasili chuoni

- Mihadhara yote itatolewa kikamilifu na kwa wakati kwa mujibu wa ratiba zilizoidhinishwa

- Orodha jumuishi ya alama za mitihani itashughulikiwa na kuhitimishwa na kisha kupelekwa kwa Afisi Kuu ya Mitahani katika kipindi cha mwezi mmoja (1) tokea mwisho wa kufanywa kwa mitihani

- Wasimamizi wa tasnifu na tafiti za uzamili na uzamifu watawapa wanafunzi wao maoni, majibu na mapendekezo juu ya kazi zao katika kipindi cha wiki mbili (2) tokea kuzipokea ripoti za kazi za utafiti au tasnifu za wanafunzi

- Kesi za nidhamu zinazowahusu wanafunzi na wafanyikazi zitashughulikiwa na kuhitimishwa katika kipindi kisichozidi siku thelathini (30) za utendaji kazi

- Chuo kitashiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba sherehe za mahafali zinafanywa kama zilivyoratibiwa katika mwezi wa Septemba kila mwaka

- Mchakato wa kuajiri na kupandisha wafanyikazi vyeo utahitimishwa katika kipindi cha muda wa miezi mitatu tokea kutangazwa kwa kazi hadi kutolewa kwa barua za uajiri au upandishwaji cheo

- Ukadiriaji wa Utendaji kazi wa wafanyikazi utafanywa kati ya mwezi wa Oktoba na Machi katika kila mwaka wa masomo

- Ununuzi wa bidhaa na huduma utafanywa katika kipindi cha wiki nane (8) kwa kuambatana na taratibu za ununuzi za Chuo Kikuu cha Nairobi na Serikali

- Chuo kitaweka na kudumisha mazingira safi, salama na ya kuvutia ya utendaji kazi

- Chuo kitakuwa **ENEO LISILORUHUSU MIHADHARATI, MADAWA YALIYOHARAMISHWA NA UVUTAJI SIGARA**

- Simu zote zitashughulikiwa katika muda wa sekunde ishirini (20)

- Mawasiliano ya kawaida yatashughulikiwa na kuhitimishwa katika kipindi cha siku saba (7) tokea siku ya kupokelewa.

- Kwa kuambatana na sera ya Chuo Kikuu, Chuo hakitaruhusu utovu wa nidhamu

- Kwa kuambatana na sera ya Chuo Kikuu, Chuo kitakuwa eneo lisiloruhusu ufisadi.

- Taratibu za kuondoka kwa wanafunzi na wafanyikazi zitashughulikiwa na kuhitimishwa kwa muda wa siku mbili (2)

- Tarehe zilizowekwa zitazingatiwa katika utolewaji wa huduma

- Chuo kitajitahidi kujenga miunganisho kati ya viwanda na wanafunzi ili kuwawezesha wanafunzi kupata kazi na ukufunzi wa muda

## UPOKEAJI MAJIBU, MAONI NA MAPENDEKEZO

- Malalamiko, pongezi na mapendekezo yatahitaji kuwasilishwa kwa Shule/Taasisi zinazohusika na kwa Afisi ya Mkuu wa Chuo.
- Majibu, Maoni na Mapendekezo yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya simu, barua, barua-pepe au visanduku vya mapendekezo ambavyo vimewekwa katika sehemu mwafaka Chuoni.
- Usiri na ufaragha wa walalamishi utaheshimiwa kila wakati
- Majibu maoni, na mapendekezo yatashughulikiwa katika muda usiozidi siku saba (7)

Zifuatazo ni anwani za barua-pepe kwa afisi kuu katika Chuo

**Mkuu wa Chuo** principal-cae@uonbi.ac.ke

**Msajili wa Chuo** registrarcae@uonbi.ac.ke

**Msarifu wa Chuo** bursar-cae@uonbi.ac.ke

**Mkuu wa Shule ya Sayansi ya Uhandisi** deanengg@uonbi.ac.ke

**Mkuu wa Shule ya Mazingira Jengwa** deanfadd@uonbi.ac.ke

**Mkurugenzi Shule ya Sanaa na Usanifu** designdept@uonbi.ac.ke

**Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi ya Nyukilia na Teknolojia** ins@uonbi.ac.ke